

REPUBLIC OF KENYA
COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THE HANSARD

Tuesday, 17th April, 2018

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 9.30 a.m.*

[The Speaker (Hon.Kahindi) in the Chair]

PRAYERS

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

NOMINEES FOR THE POSITION OF CHIEF OFFICERS

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Members, I have a Communication to make. The County Assembly is in receipt of a list from the County Secretary dated 9th of April, 2018 containing the nominees to the positions of Chief Officers. We have:-

1. Moses Gunda Munga- Physical Planning, Urban Development and Housing.
2. Mary Chari Mukare-Cooperative Development.
3. Victor Chogo Nzai-Agriculture.
4. Fredrick Baraka Kaingu- Livestock.
5. Stephen Mwakai Kiti- Fisheries.
6. Amina Nassor Abdhalla- Office of the Governor.
7. Mulewa Safari Katana- Education.
8. Eveline Mwenda Karisa- Gender, Culture, Social Services and Sports.
9. Kennedy Mganga Chilibasi- Economic Planning
10. Bilal Yusuf Mwadzoya- Medical Services
11. Alio Ibrahim Adan- Public Health.

Hon. Members, pursuant to the provisions of the County Governments Act, 2012, the Public Appointments County Assemblies Approval Act of 2017 and the Standing Orders No. 194(5) (f), the nominees are hereby committed to the respective Sectoral Committees for vetting and thereafter compile a Report to this House within the stipulated timelines.

SUPPLEMENTARY BUDGET NUMBER TWO

Communication number two; the County Assembly is also in receipt of a letter from the County Treasury dated 9th of April, 2018 submitting supplementary budget number two for the

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

financial year 2017/2018 and the accompanying legislative proposal of the supplementary budget. Pursuant to Standing Order No. 211, the supplementary estimates are hereby committed to the Budget and Appropriations Committee for consideration. Thank you.

PAPER LAID

REPORT ON STATUS OF ADU YOUTH POLYTECHNIC

Hon. Chiriba: Thank you Mr. Speaker. I rise to table a Report to this hon. House of the Sectoral Committee on Pre-Primary Education and Vocational Training on the Statement sought by hon. Stanley Kenga Karisa on Adu Youth Polytechnic. Thank you.

(Hon. Chiriba laid the Paper on the Table)

MOTION

CONSTRUCTION OF REHABILITATION CENTRES IN KILIFI COUNTY

Hon. (Ms.) Koki: Hon. Speaker, I stand on behalf of hon. Hadad Almas and I beg to move the following Motion: -

THAT, aware that drug abuse is one of the biggest problems confronting Kilifi especially youth.

AWARE THAT, incidents of drug and alcohol abuse and related anti-social behaviors have increased in recent years.

FURTHER aware that there is no single rehabilitation centre operationalized by the County Government.

NOTING with concern that the lack of a county operated rehabilitation centre has caused many youths unable to access counseling and recovery services.

This House urges the County Executive Committee Member in charge of Gender, Social Services, Culture and Sports to initiate measures for establishing three County rehabilitation centres at Mtwapa, Kilifi Town and Malindi.

Thank you. Mr. Speaker, Sir. Drug abuse among our youth has led to a lot of risky behaviors leading to early pregnancies, HIV and AIDS. It has also led to neglect. If you look at the society, people who use drugs are neglected; they are shunned by the society because they are deemed as useless people in the society. This has also led to poor relationships with their parents. Drugs have also led to a lot of crimes like theft, violence, rape e.t.c. It has also led to death. We have seen them being beaten to death because they have stolen. What they need is to get money and they are not working; they can't help themselves financially so they will go to steal and get money for the drugs.

This menace is growing time after time here in Kilifi County and I think it is high time to stop this. With those remarks, I will call upon hon. Nuzla to second the Motion.

(Hon. (Ms.) Nuzla seconded)

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.

(Question proposed)

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes hon. (Ms.) Nuzla.

Hon. (Ms.) Nuzla: Asante Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa kama hii. Kama tunavyojua, ndani ya Kaunti yetu vijana wameathirika na dawa za kulevya na nikisema vijana wameathirika si kuwa ati nachangia waendeleo kutumia kwa sababu tunataka hizi sehemu ambazo wataweza kwenda kujisaidia na dawa pale. Ni kuwa tunasema mtoto akinyelea paja huwa halikatwi; huwa linaoshwa na mtoto akabebwa vizuri. Kuna changamoto kubwa sana kwa hii Kaunti. Mwaka jana kuna vijana kutoka Watamu ambao walikuwa wamejiingiza katika dawa hizi za kulevya na wako tayari kujitoka katika hizo dawa lakini dawa za kuwasaidia ndani ya Kaunti ya Kilifi ikawa ni changamoto kubwa kupata.

Mimi nakumbuka vijana kama wale walijiunga kwenye makundi na wakanifuata kuniambia sisi tunataka kwenda Malindi kufuata dawa lakini hatuna hata nauli ya kufikia huko. Nikaongea na Idara husika na wakasaidiwa na gari wakafika Malindi lakini kukawa bado kuna changamoto ya kwenda asubuhi na kurudi jioni. Mara nyengine wanaambiwa hata pengine dawa ni saa nane, kwa hivyo ikawa ni changamoto kubwa kwa upande wao.

Ukienda Mtwapa shida ni hizo hizo. Mtu atoke Mtwapa mpaka Malindi kufuata dawa. Kwa hivyo, itakuwa ni jambo zuri na la busara hii Idara wajenge sehemu za kuwasaidia hawa vijana. Ikiwa hatutaweza kufanya jambo kama hili ama kupitisha ndani ya hili Bunge, basi katika miaka ijayo vijana asilimia 90 watakuwa wameathirika na dawa za kulevya na kutupotezea wakati wetu na hatutaweza kuwasaidia hao vijana.

Tunaambiwa upatilizie udongo ungali maji; japo twajua ndani ya Kaunti ya Kilifi, vijana walioathirika ni wengi lakini haijafikia asilimia 70 na hatutaki ifikie hapo na ndio maana tunasema ya kwamba ni muhimu kujengewa maabara ya vijana wetu kwenda kusaidika katika hizo sehemu. Ikiwa pengine halijakupata wewe ama jirani yako, basi labda mtoto wa jirani yako limempata. Mimi naomba waheshimiwa wenzangu, tuunge mkono jambo hili ili tusaidie vijana wetu. Hatusisitizi waendeleo kutumia dawa za kulevya, lakini wakiwa sehemu kama zile watapata maono mengi na huenda kijana kama yule apunguze maanake ndani ya hii Kenya, kuna viongozi ambao walikuwa wamejiingiza katika dawa ya kulevya leo hii ni mawaziri leo hii ni marais wa Kenya.

(Laughter)

Kwa hivyo, mheshimiwa Spika, najua hapa pia kwetu tunao lakini hatusisitizi sana. Kwa hayo machache, waheshimiwa wenzangu tusimame na kuchangia Mswada huu. Asanteni.

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes hon. Stanely Kenga, proceed.

Hon. Kenga: Asante sana mheshimiwa Spika kwa nafasi niliyopata ili niweze kuchangia Mswada ambao uko mbele yetu. Mimi naunga mkono Mswada huu kwa sababu zifuatazo. Kwa mjibu wa Katiba ya mwaka wa 2010 ratiba ya nne na kifungu cha 13 inaeleza majukumu ambayo serikali zetu za Kaunti zimepewa ili kuweza kuhudumia wananchi na moja ya yale majukumu ambayo tuko nayo ni mambo ya dawa na maswala ya ngono. Hizi ni changamoto ambazo Kaunti zetu zinapatia.

Ni kweli kwamba vijana wengi, kuna wale wa umri mkubwa na kuna wale wa umri mdogo ambao wamejiingiza katika maswala haya na wameweza kuathirika na athari zile zikawa na mguso kwa jamii nzima ya watu wa Kilifi. Kama Serikali, ni lazima kuwe na mikakati

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ambayo itatoa suluhisho mwafaka. Njia moja ukiangalia ombi la Mswada huu ni kwamba kuwe na vituo ambavyo vitajengwa na vituo vile viweze kuwa na dawa, mashauri na mambo kama hayo.

Wale ambao wemejiingiza na hali hii watakuwa na nafasi ya kuweza sasa kuanza kupata msaada. Mimi leo nimefurahi sana kutoka kwa mheshimiwa ambaye ameunga mkono Mswada huu ambao tumejadili kwamba hata marais katika jamhuri yetu ni miongoni mwa viongozi ambao wamepitia maswala haya lakini kwa mikakati kama hii iliwekwa wakaweza kumakinika na kupata nafasi ya kuongoza taifa letu la Kenya. Hii inatupatia picha gani? Kwamba kuna vijana, watoto wetu na ndugu zetu ambao bila shaka wako na ndoto, wako na nyota na iwapo nyota ile tutaipalilia...

The Spekaer (Hon. Kahindi): Yes hon. Kiraga what is your Point of Order?

Hon. Kiraga: Asante sana mheshimiwa Spika. Ningeomba mnenaji ajaribu kudhibitishia Bunge hili yale ambayo anaongea ya kwamba rais wa jamhuri hii ya Kenya alikuwa miongoni mwa haya ambayo tunazungumzia hivi leo. Ningeomba sana athibitishie Bunge hili.

The Spekaer (Hon. Kahindi): You know hon. Stanely Kenga; do not forget the handshake... the President now has people to defend him here.

Hon. Kenga: Kabla hatujaangalia maswala ya kupeana mikono nadhani mheshimiwa Peter Ziro, sijui kama yuko hata yeye ali *extend handshake* na mheshimiwa Fondo wa Garashi. Kwa hivyo, haijamaanisha kama kuna Mswada...

The Spekaer (Hon. Kahindi): What hon. Kiraga is asking is you substantiate or you simply withdraw because it is very bad for the record. I do not think we have any evidence to show that.

Hon. Kenga: Ili nipate nafasi ya kuweza kuchangia zaidi pengine naweza omba nafasi ili niweze kuyadhibitisha zaidi. Sijaomba, lakini naweza omba nafasi. Naweza sema hivi, mheshimiwa Kiraga uliona wakati Jaji Maraga alipotangaza kwamba ni lazima uchaguzi urudiwe na viongozi wawili wakaweza kukutana wakaanza kuhutubia nchi, uliona jinsi ilivyokuwa?

The Spekaer (Hon. Kahindi): Yes hon. Stanely Kenga you are out of Order! Just conclude with your statement.

Hon. Kenga: Mheshimiwa Spika naomba *ku withdraw* sijui kwa Kiswahili nitasemaje?

The Spekaer (Hon. Kahindi): Thank you, proceed.

Hon. Kenga: Na nipewe ulinzi ili niweze kuendelea. Sasa nilikuwa nasema kwamba ndani ya taifa la Kenya kuna watu mashuhuru ambao wamehusika na dawa za kulevywa lakini wakati walipohusika hawakuwa mashuhuri. Lakini walipopata nafasi ya kurekebisha wakatolewa katika kundi lile la mashaka na walipotolewa wakapata nafasi ya kunawiri na ndio leo tunasherekea kwa nafasi walizonazo na mifano ipo japo inapotajwa wengine wanahisi wameguswa visivyo. Kwa hivyo, tutabana hatutataja lakini kwa mifano hiyo tuko na kila sababu... Idadi kubwa ya wananchi wa Kilifi wako katika umri ule wa vijana na tusipowawekea mikakati, tunamaanisha kizazi tunapoteza na tunapopoteza kizazi, ni hasara kubwa ambayo kama watu wa Kilifi tutakuwa tumeweza kuipata. Kwa hivyo, mimi naunga mkono mikakati iweze kufanywa kikamilifu na mheshimiwa Kiraga ni shahidi wa maswala ninayoyazungumza.

Unajua tukiwa nje tukizungumza, mimi na yeye akiwa rafiki na jirani huniambia haya maswala. Kwanza hata ninapozungumza nachangia kwa sababu najua yeye wakati fulani aliweza kunithibitishia...

(Laughter)

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.

Na kule kwake Gongoni eneo letu jirani hapo Mambrui kuna mtaa wa Ngomeni ambao uko kwake, hata kwangu Marereni hawa vijana tunawapata mitaani ambao wameathirika. Tukiwa viongozi, ni lazima tuwe na mbinu na mikakati. Nampongeza mheshimiwa aliyeleta Mswada huu nauunga mkono kikamilifu na ombi langu ni kwamba sote tukiwa viongozi tutashirikiana kuhakikisha kuwa hili limefanyika na vijana wetu wamepata nafasi ya kushauriwa, kurekebisha na kupewa tena nafasi nyingine ili waweze kutambua ndoto zao. Bila shaka, Mwenyezi Mungu anapowasaidia wawe viongozi bora kama wengine walivyoathirika na hatimaye wakaweza kurekebisha na wakaweze kuwa watu wa manufaa katika jamii. Kwa hayo, naomba kuunga mkono.

Hon. (Ms.) Maneno: Asante sana Bw. Spika kwa kunipatia fursa hii. Nimesimama kuunga mkono Mswada huu. Ukiangalia Mswada huu, umeletwa kwa wakati ufaao haswa wengi wakiwa ni vijana katika hili Bunge. Ni kweli vijana wetu wanapotea kupitia mihadarati; ninaunga mkono kujengwe hivi vituo na hivi vituo si vijengwe tu, yule aliyeathirika aende kule asubuhi na jioni, la hashu! Ni vituo vijengwe na viwe na mabweni.

Nimebahatika kupata nyumba ambayo iko karibu na hospitali yetu kubwa ya Malindi na huwa ninaona hao vijana asubuhi wanapita lakini baada ya saa mbili ama matatu wanaenda kupata dawa. Wanaenda kule wanakoenda wanakaa pamoja wanarudia tena tabia ya kupata zile dawa. Sasa tunaona ya kwamba hapa hatuwasaidii ndiposa ni lazima vituo vijengwe viwe na mabweni. Mtoto wako ukimpeleka pale awe anapata ushauri ambao unastahili na baada ya muda, yule ambaye atakuwa ameruhusiwa kukaa pale akitoka, basi tutakuwa tunategemea huyo kijana. Lakini tukisema hivi vituo vijengwe na viwe ni aende asubuhi jioni arudi ule wakati wa mchana wote tutakuwa tunajua anafanya nini? Kwa sababu akitoka kule hataenda nyumbani kukaa, ni lazima atajiunga tena na yale makundi ya wale vijana.

Na wengine ni vijana wazuri wameingia tu kwa hii tabia kupitia kwa vijana wengine. Mimi mwenyewe nina mtoto wa dadangu amepitia haya. Nasema hivyo kwa sababu tulimpeleka katika bweni Shika Adabu upande wa Mombasa ndio kwenye hiyo *rehabilitation center* lakini tulilipa shilingi 120,000 na baada ya hapo, mototo amerudi Kaloleni yeye amekuwa sasa ndiye mkubwa wa kufundisha wenzake. Lakini wale ambao wako na ari, wale ambao wanataka kubadilika tukiwapeleka pale ni lazima watabadilika. Bw. Spika, kwa hayo machache nimesimama kuunga mkono Mswada huu.

Hon. (Ms.) Radhia: Asante mheshimiwa Spika. Kwanza, utanisamehe kidogo niko na mafua. Mimi nimesimama kuunga mkono Mswada huu. Kwa vile mimi ni mzazi nimepitia mengi na nimeona mengi, hususan nikitoka katika eneo la Shella ambalo kila mmoja analitambua kwa sifa hiyo ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, hizi dawa za kulevya katika Kilifi Kaunti ama nikisema Pwani nzima ni ugonjwa mkubwa kushinda Kaunti nyingine. Tunasikitika sana kama wazazi kuona vijana wetu wako mabarazani na uhalifu wote unasababishwa na dawa za kulevya. Na tukisema dawa za kulevya nina hakika sote tunajua kuna mengi lakini kuna haya ya saa hizi ambayo yamejitokeza ndio athari kubwa kwa wototo wetu.

Kama wenzangu walivyochangia kwamba vituo vijengwe na wengine wamezidisha kusema viwe vya mabweni, lakini ni kwamba tuangalie kwanza *Bismilahi*, kwa hiki ambacho kiko, je kimeleta natija gani kwetu? Halafu turudi tuangalie tena nyuma tukiangalia ni kitu gani kinasababisha watoto wetu waende katika mihadarati? Vituo tutajenga na je, baada ya kujenga hivyo vituo, kuna natija gani tutapata katika hivyo vituo? Vituo nasisitiza vijengwe lakini kuna

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mambo ambayo lazima tuangalie katika hivyo vituo kwa sababu vituo viko na dawa za kulevya hapo hapo ndani zinatunika. Vituo vipo na ndani ya hivyo vituo, dawa za kulevya wanapelekwa na ndio nafuu kwa wale wanaojenga hivyo vituo. Wasipovuta dawa watoto, vituo vitafungwa.

Badala ya kuwa usaidizi mheshimiwa Spika, imekuwa kila anayetoka anakwenda akirudi, natija tunazozipata ni kidogo nafuu kwa wachukuzi wenye kujenga hivyo vituo. Kwa hivyo, mheshimiwa Spika, ningependa tuwe makini baada ya hivi vituo kujengwa tuweke mikakati na pia tuangalie kazi muhimu kwa vijana. Mtoto ameenda pale amejirekebisha kwa wale wanaotaka kujirekebisha akitoka hana kazi, wataka afanye nini zaidi ya hapo asiregee kwenye dawa za kulevya? Mimi naomba wenzangu waniunge mkono tupange mikakati ili tujue vijana watapata vipi kazi katika Kaunti yetu ya Kilifi. Bila ya kupata kazi, vituo havitasaidia. Mtoto ataenda kituoni atakaa miezi yake mitatu atarekebishika akirudi huku hana kazi atawaona wale wenzake ambao hawajaenda atarudi pale pale kama mheshimiwa Maneno alivyosema.

Pale kwangu tuko karibu na mheshimiwa Maneno asubuhi wakirudi hawana kazi wanarudi maskani; kule wanakunywa dawa mtaani wanarudia uraibu wao. Nikisema hivi, nina huzuni moyoni mwangu kwa sababu vijana wengi pale mtaani kwangu ninapokaa, kila nyumba mtoto mmoja ama wawili wameharibika kwa dawa za kulevya. Kama wako hajaharibika lakini hakikisha unamgandama.

Mimi mwenyewe nakaa naye pale yukochuo kikuu na akirudi simuachi kwa sababu najua nikimuachilia tu kidogo atajisahau na wale ni wenzake wamekua na wao hakuna budi ataongea na wao atakaa maskani na kitakachofanyika ni kutumia dawa za kulevya. Naomba waheshimiwa wenzangu sote tushughulikie Mswada huu wa mwenzetu aliouleta katika Bunge hili kwa wakati uliofaa. Vituo vijengwe lakini nasisitiza kazi kwa vijana; bila kazi vijana watarudi maskani tupende tukatae.

Naomba mheshimiwa Spika, hususan kwa wale waliojirekebisha wameenda kwenye vituo viko ama vitavyokuja tukiwaona wamejirekebisha ni lazima ama muhimu kijana kama yule apatiwe kazi, awe ni mfano kwa wengine. Lakini ukiongea na vijana, wanasema kweli mama tunaenda twataka kutibiwa lakini tukirudi hatuna kazi tutafanyaje? Nasisitiza nikisisitiza kijana aliyejirekebisha naomba afanyiwe kivyovyote kijana kama yule kutoke nafasi za kazi kwa wale vijana waliojirekebisha. Kwa hayo machache, nashukuru sana mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi kama hii na naunga mkono mia kwa mia Mswada huu.

Hon. Changawa: Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii ili kuchangia Mswada ambao uko mbele ya Bunge hili. Nataka niseme kwamba nimesimama kuunga mkono Mswada ambao uko mbele yetu mia kwa mia. Waswahili walisema kwamba mtoto wa mwenzako ni wako na mui huwa mwema. Walikuwa wameyaona ya kwamba kile kibaya kiko na nafasi ya kubadilika na kuwa na thamani kwa siku za usoni.

Naunga mkono kwa kujengwa vituo hivi vya urekebishaji tabia kwa hawa ndugu zetu ambao wamepotea katika kutumia kile ambacho hakistahili kutumika. Mimi mwenyewe binafsi nasimama kusema kwamba kama kuna mengi ama mambo yalionyichangia kuingia katika hili Bunge nafikiri jambo hili la kushughulikia watu hawa lilikuwa sababu ya mimi pia kuweko katika hili Bunge.

Mheshimiwa, kuna kijana kabla wakati wa kura alitamani sana kusaidiwa akiwa jirani ya mheshimiwa George Baya pale Watamu na kijana huyo alinifuata katika kutafuta kura zangu na kutaka kusaidiwa ili kuacha utumiaji wa dawa za kulevya. Nilijaribu pale nilipoweza ikiwa ni

kigezo pia cha kutafuta kura lakini mpaka hivi leo, amekuwa wa manufaa katika boma lao. Kwa sababu, kweli ameacha na yale ambayo anayafanya katika lile boma, hakika mui hua mwema.

Nataka niseme ya kwamba kama kuna mambo ya muhimu ndani ya Kilifi ambayo ni tuyafanye ni mambo kama haya na kujenga vituo hivi. Haimanaanishi ya kwamba tunachangia watumiaji dawa za kulevya wawe wengi, lakini sawa na vile mbavyo hukaa na kujenga vyumba vya kuhifadhi maiti si kwamba tunataka watu wafe, sawa na vile ambavyo kujenga hospitali si ati tunataka watu wawe wagonjwa lakini wale watakaokuwa wagonjwa wawe na mahali pa kusaidika. Wale watakaoga dunia wawe na mahali pa kuwekwa kabla ya kuzikwa. Hivyo nasema ya kwamba vituo hivi vijengwe ili wale walioathirika, wale watakaathirika na wale wanaoendelea kutumia wawe watasaidika kupitia kwa vituo hivi.

Nasema ya kwamba nikiwa karibu na jirani yangu Mheshimiwa George Baya si Malindi tu; tunasema Watamu iko na jina kubwa maana hata aliyeamua anakuja Kilifi jina la kwanza atakalolisikia ni Watamu kabla hajasikia Malindi na Kilifi. Kwa hivyo, nasema Watamu pameathirika na ni mahali pa wageni. Vituo hivyo vitasaidia watu wetu. Nashukuru kwa nafasi hii lakini nasisitiza ya kwamba vituo hivi vijengwe ili visaidie watu wetu. Asante.

Hon. Maitha: Asante Mheshimiwa Spika. Nami nasimama kuunga mkono Hoja hii. Nishawahi kufanya kazi na shirika la kibinafsi ambalo lilikuwa linaangazia utumiaji wa mihadarati; ni changamoto kubwa na swala hili ni kubwa linataka uangalifu wa hali ya juu. Ninaunga kono kujengwa kwa hizi sehemu za urekebishaji. Kama wenzangu walivyochangia wamesema ya kutosha na ninaweza kupeana mifano kama mwenzangu anayewakilisha Mnarani. Tulikuwa tunafikiri mihadarati inatumika tu kwa hii miji lakini Mnarani pameingiliwa na utumiaji wa mihadarati; imeanza kusambaa na kufikia hata Jaribuni. Kwa hivyo, kituo hiki kikiwa Kilifi kitatusaidia kwa njia moja ama nyengine.

(Hon. Kenga rose on a Point of Information)

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes hon. Masha (Maitha), do you wish to be informed by hon. Stanley (Kenga).

Hon. Maitha: No!

The Speaker (Hon. Kahindi): Proceeded.

Hon. Maitha: Akiwa rafiki yangu kwa leo naomba atulie kidogo. Jambo hili la miharadati tulipe nafasi ya kulichunguza kwa kina kwa sababu vijana wetu huwa wanaanza wakiwa na umri mdogo. Leo hii ukienda kwa hizi sherehe zinazojulikana sana kama *usiniriche* utapata vijana wetu wanaanza pole pole kutumia *mogokaa* na wanapanda pole pole; saa hii wanatumia ugoro na mengineyo na inafikia mahali pa kutumia unga (*cocaine*). Nilishangaa nikifanya kampeni kijana aliyekuwa kidato cha kwanza shuleni miaka hiyo ya nyuma ananiita “mwanangu” sasa nikashindwa. Nikashangaa kijana mdogo vipi niwe mtoto wake? Lakini yote nilivyoona ni kwamba kijana aliacha kazi Mombasa Kilindini lakini kwa sababu ya mihadarati ikabidi aache kazi na aendele kutumia dawa zile.

Swala hili ni kubwa kwa sababu nilikuwa nikifikiri vijana wanatumia mihadarati kwa sababu hawana kazi, lakini wakati nikiishi pale Barisheba nikifanya shughuli na hili shirika la kurekebisha wale wanaotumia mihadarati ni kwamba tulikuwa tunajaribu kuangalia kama ni kweli hawana kazi ndio wanatumia mihadarati. Je, wakipata kazi na misharaha si ndio watakuwa na pesa zaidi za kununua mihadarati? Kwa hivyo, hili jambo si la kuangalia tu sehemu moja ya kwamba vijana wetu wanatumia mihadarati kwa sababu hawana kazi; tuangalie kwa undani

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wapewe ushauri ambao utawasaidia maishani mwao. Ni jambo ambalo naliunga mkono, sehemu kama hizi zijengwe na bado tuchukue nafasi ya ndugu zetu wale ambao walisomea *counseling* ili wawe watapeana ...

Hon. Kenga: Mr. Speaker, is the hon. Member for Jaribuni Ward in order to make contributions to this very important Motion without disclosing that he is a qualified Doctor? We have two Doctors in this assembly; Dr. Kiraga and Dr. Maitha and because this issue touches on the issue of professionalism and especially on medicine, I think it is important that he goes on record that he is a Doctor and what he gives is his professional contributions regarding the Motion that is before us. Thank you.

The Speaker (Hon. Kahindi): I overrule that. Kindly proceed.

Hon. Maitha: Asante kwa kunitetea Bw. Spika. Nasimama hapa kama Mwakilishi wa Wadi ya Jaribuni. Naunga mkono Hoja hii.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you.

Hon. Baya: Thank you Mr. Speaker, Sir. I stand here 100 percent in support of the Motion. This Motion is touching on me personally as the MCA (Member of County Assembly) representing Watamu Ward. What is happening in Watamu is a disaster; talents, lives and opportunities are in danger. I arrived here late because I had to take some of the boys to Malindi General Hospital for rehabilitation. They found me on the road and they said they did not have bus fare to get to the hospital.

An incident happened last week where a boy met an Italian lady; she gave him one million shillings and in one week, the boy was found in hospital and he could not even afford a bill of Kshs10, 000 because he had finished the million shillings. He couldn't even explain how the money got finished.

I, hon. George Baya Mramba *aka* Tandoori, representing Watamu was once a victim' a long time ago when in was still in school. I was abusing drugs but thank God I got born again and Jesus saved my life. Now you can see what I am contributing in this House and the people of Watamu have confidence and faith in me. So, I support this Motion that rehabilitation centres must be built and we get at least one branch in Watamu Ward because Malindi is a bit far from Watamu since most of those boys come from Watamu while for now, Malindi is almost safe but Watamu is in danger Mr. Speaker, Sir. Thank you.

Hon. Mae: Asante mheshimiwa Spika. Mimi nasimama kuunga mkono. Nimewahi kukulia katika sehemu ambayo ilikuwa sana na shida hii ya mihadarati na kwa wale vijana ambao tulianza shule pamoja naweza sema asilimia 99 wameweza kupoteza mwelekeo kwa sababu ya hii mihadarati. Lakini kikubwa tusiangalie tu juhudi tu za kujenga hizi sehemu za marekebisho. Sisi kama Kilifi naweza sema zamani tulikuwa tunasikia tu kwamba kuna mihadarati lakini sasa mihadarati imeingia Kilifi. Tumeambiwa Malindi, Watamu, Kilifi mjini na sasa mihadarati hii imeanza kupenya kule kwetu mashambani.

Mheshimiwa Spika, kama hatutakuja na michakato ya kujaribu kuzuia mihadarati hii isiuzwe hapa Kilifi, tutakuwa tunajenga... waswahili wanasemaje? Kujenga ukuta ama ni ufa? Unajua Kiswahili kina wenyewe. Tutakuwa tunaziba ufa badala ya kujenga ukuta. Sasa tuangalie kuzuia ndio naunga mkono kujengwa kwa hizi sehemu lakini kuzuia. Ni kina nani hawa watu wanatuuzia hii mihadarati? Hii mihadarati inauzwa wapi? Kwa sababu sote tunajua kuna watu mitaani tunawajua kuwa fulani anauza, lakini kama tutajenga sehemu za kurekebisha tabia halafu yule gwiji wa kuuza mihadarati ile tumemuacha pale, mimi naona tutakuwa tunampigia mbuzi gita kwa sababu kama vile tumesikia mheshimiwa Radhia, vijana wataenda kule vituoni halafu

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

baadaye kwa kuwa yule gwiji yuko mtaani, bado vile vile watarudi pale. Kwa hivyo, serikali ya Kilifi inatakikana kujizatiti kuona kwamba mihadarati hii haiuzwi hapa Kilifi. Najua wenye kuiuza ama wenye kuileta ni watu wenye ushawishi mkubwa katika serikali lakini kama Kilifi, sisi pia tuliona mwaka jana kule Kiambu wakati kina mama wamejifunga kibwebwe wakimwaga zile pombe na kuleta vurugu kule. Lakini je, hapa kwetu sisi kama watu wa Kilifi, kina mama zetu tunaweza tukatoka kwa pamoja tukijua huyu mtu anauza mihadarati na tuende pale kama ni kuharibu tuharibu kama wale wenzetu wa Kiambu walivyofanya?

Mimi binafsi nimechukua hatua fulani kupambana na jambo hili. Mimi hatua zangu nimezielekeza kwa kina dada. Mara nyingi huwa nina tabia ya kuingia kwenye vilabu, si kwamba kuingia ili kustarehe, mimi mara nyingi huenda kuingia... na unajua unapokuwa kijana mtanashati unapoingia sehemu kama zile unakuwa dhahabu; unakuwa lulu. Kwa hivyo, huwa huchukui mda huwa kuna watu wanakuandama sasa mimi huchukua nafasi ile anayeniandama kwanza mimi hutaka kujua kwa nini umeingilia shughuli hii ya kujiingiza kwa maisha haya kwa sababu wale wengi ukiwapata vile vituko wanavyofanya, huwa hawavifanyi wakiwa macho makavu bali kuna vitu wametumia ndio unapata anakuja kufanya vituko vilivyo tofauti. Sasa unapata mtu amekuja pale kama mteja lakini unapomleta pole pole anakuja unajua ni sababu gani yuko pale. Nimewahi kuokoa maisha ya wasichana watano kufikia sasa na nimewatoa katika hali ile na kutumia hela zangu za mfukoni. Kwa nini wewe uende kufanya mambo kama yale? Je, ni kitu gani kingine unaweza ukakifanya?

Mheshimiwa Spika, najivunia kwa sababu kuwatoa wasichana watano katika hali ya mihadarati na bila kuwadara unajua...

(Laughter)

inataka roho kwa sababu sisi kama wanaume wakati mwengine tuna...

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes hon. (Ms.) Nuzla? Una Hoja ya Nidhamu, ama?

Hon. (Ms.) Nuzla: Niko na Hoja ya Nidhamu. Mheshimiwa Spika, naomba atueleze itakuwaje yaani wasichana watano peke yake ndani ya vilabu kama hivyo na uwatetee wasichana peke yao usitete wavulana pia? Hapo pamenishangaza. Halafu pia, naomba mheshimiwa ajieleze vizuri yaani bila ya kuwadara ki vipi? Hapo pamenishangaza kiasi.

Hon. Mae: Mheshimiwa Spika, mimi nimesema nilichukua muelekeo wa kutetea wasichana; watoto wa kike. Na sijamfungia mheshimiwa Nuzla yeye naye kuingilia kutetea watoto wa kiume kwa sababu nimetangulia kusema kama kijana unapoingia kwenye eneo la starehe...

(Laughter)

The Speaker (Hon. Kahindi): Just proceed we have understood your point hon. Member.

Hon. Mae: Najaribu kumueleza dadangu hapa. Kama kijana, unapoingia kwenye kumbi za starehe mtu wa kwanza kukuandama huwa ni msichana si kijana mwenzako. Kwa hivyo, jukumu hilo ndio nikaona wacha nielekeze nguvu zangu kwa hawa kina dada...

(Hon. Changawa stood on a Point of Order)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Changawa: Naomba mheshimiwa aliyekuwa jukwaani atuelezee, kijana ni mwanamume ama kuna kijana wa kike na wa kiume kwa sababu anatupotosha.

Hon. Mae: Asante. Pengine Kiswahili kina wenyewe na mara nyingi mimi hutumia lugha ya Kiingereza sasa leo nimesema wacha nikuze lugha ya Kiswahili sasa endapo kidogo nitatoka nje, ni vizuri kunirekebisha. Mimi nguvu zangu nimeweka kwenye vijana wa kike. Na mheshimiwa Spika, nafikiri hoja zangu mbili ambazo nimezitilia mkazo ni kwamba naunga mkono na hata kama naunga mkono kujengwa kuwe na mchakato wa kuweza kuzuia dawa hizi zisiweze kuuzwa hapa Kilifi. Kwa hayo mengi na machache nasema asanteni.

(Applause)

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you.

Hon. Mwayaa: Asante sana mheshimiwa Spika. Nami nasimama kuunga mkono Mswada wa vituo vijengwe katika Kilifi yetu kwa ajili ya urekebishaji wa wale wanaotumia mihadarati. Bunge lile la kwanza niliwahi kuwa na tulifanya mikakati na siku moja Kamati ya Afya ilitembea sehemu za Msabaha na kutembelea kituo ambacho kilijengwa pale lakini ni cha mtu binafsi. Malengo yetu hasa katika lile Bunge la kwanza ilikuwa ni kuja na mikakati na tuone vile ambavyo yule mtu binafsi alivyojenga kituo chake ili kwamba sisi pia kama Kaunti ya Kilifi tuweze kuja na mikakati ya vituo kama hivyo.

Aliyeleta maono haya namuunga mkono kwa sababu maono yamekuja kwa wakati wa sawa ili kwamba akanikumbusha yale ambayo tulifuatilia. Wakati huo tulikuwa na daktari Kiraga kama mwenzangu alivyosema hapa, lakini wakati ule tulikuwa na daktari mmoja. Saa hii kwa vile *Deputy Speaker* alisema ni wawili, nafikiri utaalumu umezidi katika hili Bunge tutaendelea mbele tuweze kujenga vituo vile. Nikiunga mkono mheshimiwa Cantona Mae alivyosema, yeye ame *specialize* kwa wasichana labda kutatokea mwingine ambaye ata *specialize* kwa vijana wa kiume. Lakini naomba pia tuje na mikakati kwa sababu ukitaka kukomesha siafu kurandaranda ni utafute mahali anatoka na uzibe. Kwa hivyo, tutafute na tuje na mikakati ili tuzibe hizi njia ambazo zinatumiwa kuleta hizi dawa za kulevya hapa Kilifi.

Mheshimiwa Spika, juzi kulitokea haya mambo ya makaa ambayo kwa sasa hivi wale askari ambao wako kwa barabara hawaruhusu makaa kupita. Kinachoharibu watoto wetu ni mihadarati na tumeshindwa kudhibiti. Tunaelekea wapi kama serikali wakati makaa tumeshuhudia Kaunti nyengine zikichoma magari yanayobeba makaa?

Mihadarati inaingizwa katika Kaunti yetu na inaharibu vijana wetu. Serikali yetu ya Kaunti iangalie mahali kunatoka hiyo mihadarati na tudhibiti hali hiyo. Tujitahidi kujenga hivi vituo lakini pia tujitahidi kuziba hizi njia zinazotumiwa kuleta mihadarati na kuharibu watoto wetu. Naunga mkono vituo vijengwe na watoto wetu waweze kuishi kwa usalama. Asante.

Hon. Kiraga: Thank you very much Mr. Speaker. I wish to contribute in support of the Motion. First and foremost, let us understand what drug abuse is. If everybody could understand the meaning of drug abuse you would realize almost half of us here might have abused a drug. There are two categories of drugs; we have pharmaceutical drugs and non-pharmaceutical drugs. What is mostly being abused, Mr. Speaker, are the pharmaceutical drugs and these are biological terms very few might understand. These drugs have also been categorized as solid and liquid drugs...

(Loud consultations)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Speaker (Hon. Kahindi): Let us give him time to explain their language...

Hon. Kiraga: Mr. Speaker, if you visit a doctor and you are given a dose of paracetamol to take two tablets in the morning, two in the afternoon and in the evening. When you take two in the morning and skip in the afternoon then you are abusing that drug and you are a drug abuser. If ...

(Hon. Changawa stood on a Point of Information.)

I do not want to be informed. If it is a matter of injections, Mr. Speaker, you are given two injections per day; if you skip one injection you are also abusing that drug. That is why I have said in one way or the other, some of us might have abused drugs.

(Hon. Changawa stood on a Point of Order)

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes hon. Changawa what is your Point of Order?

Hon. Changawa: Asante Mheshimiwa Spika. Nataka kumuelekeze mwenye yuko mbele kwamba Mswada ambao uko hapa ni wa kujenga vituo vya wale walioathirika na madawa ya kulevya. Haijalishi ni dawa alikosea kumeza kulingana na maagizo ya daktari na ikamuathiri. Jambo ambalo tunazungumzia ni kujenga vituo vya wale walioathirika iwe ni kwa dawa za kulevya ama za hospitali. Yale anayoongea itabidi wataalamu wafike. Kwa hivyo, nataka tu atuelekeze ama aende katika ile...

(Hon. Changawa spoke off record)

The Speaker (Hon. Kahindi): I concur with you hon. Emmanuel (Changawa). Yes hon. Kiraga just focus on the context.

Hon. Kiraga: Thank you very much. Mr. Speaker. Everything must have an introduction and in fact if you want to build a house you do not just wake up and start building; we have what we call planning stage.

(Laughter)

The Speaker (Hon. Kahindi): I have understood the introduction so let us go ...

Hon. Kiraga: Thank you very much. Most of the highly abused drugs are the sedative drugs Mr. Speaker. When we talk of sedative drugs, we are talking of the Intravenous Drug Use (IDU) and the IDUs form part of a very big percentage of the drug usage in this country. The drug usage has become a hobby in this country and it is very dangerous.

Mr. Speaker, we cannot separate drug usage and HIV/AIDs prevalence. I brought this introduction so that Members can now appreciate the magnitude of this problem we are having. The prevalence rates as far as HIV/AIDs is concerned, in Kilifi County currently is at 4.6 percent and at 5.7 percent country wide. As a County, you can gauge where we are. We are treading on very dangerous ground, and if you look at this rate, it has been contributed by the drug usage.

Mr. Speaker, some hot spots have been highlighted; Watamu, Shella, Ngomeni, Mamburui and of late Gongoni and Marereni. In 2015, if I am not mistaken, a research was done and

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Watamu was the hottest spot in Kilifi County as far as drug usage is concerned and even the prevalence rate, by then, Watamu as a village was leading.

If we have these centres and I concur with hon. Amina, hon. Mae and the other Members that it is not a matter of building these centres but equipping them and we should also have capacity building for these people to ease the situation. I have been cautioned by hon. George Baya that I use light words but I am to go to my last words of my contribution. I think some of you might ... so let me end up here.

(Laughter)

Hon. (Ms.) Ngari: Asante sana Mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono Hoja hii. Nataka kusema labda hata Hoja hii watu wamesema imekuja kwa wakati lakini tuseme imechelewa na kama haijachelewa, serikali labda ndio imechelewa maanake vijana wetu wameanza kitambo sana kutumia mihadarati na kila uchao wanaongezeka na kusema kweli, serikali haijachukua hatua mwafaka ya kuhakikisha kwamba vijana hawa ni mbinu gani watahakikisha kwamba wameacha mihadarati.

Mashirika yasiyokuwa ya serikali yamejaribu sana kuona kwamba vijana wameachana na hizi starehe za mihadarati na huwa wako na mbinu ambazo hazitibuki. Mbinu zao wakizitumia wanahakikisha kwamba zimewaondoa vijana wale kutumia mihadarati japo hawajaweza kufikia vijana wengi kwa sababu huwa wamekuja kikazi na huwa wana lengo ya kwamba wanahitaji vijana kadhaa ndio waweze kuwabadilisha. Nimesimama kuunga mkono kujengwa kwa vituo hivi na kusema kwamba vijana hao ambao watakuwa wameenda kwa vituo hivyo na wakitoka hapo wako sawa hawana kazi labda hapo tutafakari maanake tukiwa hapa, tunavyo vyuo vya ufundi ambavyo vinajengwa katika maeneo yetu kwa kila wadi na vituo vile kusema kweli, havijapata vijana wa kutosheleza kusomea nafasi hizo za taaluma.

Mimi naona kazi ziko isipokuwa ni sisi tutafakari sote kwa pamoja ni mbinu gani za hamasa ambazo zitawawesha vijana hawa kujiingiza katika vyuo vya ufundi ili waweze kunufaika na kujijiri. Maanake kazi si mpaka ajira. Tukisema tunataka kuajiri hawa vijana wote nafikiri nafasi hizo za kazi hazitaweza kupatikana isipokuwa wakijifundisha, wakiwa na ujuzi wenyewe wanaweza kujijiri. Kwa hivyo, mimi naunga mkono sana kujengwa kwa hivi vituo na sio kwamba vituo hivi vikijengwa havina mbinu, ni lazima vijengwe na vitakuwa na mikakati ya kuhakikisha kwamba watoto wetu wametoka katika mihadarati. Ikiwa ni vituo vijengwe bila mikakati, basi labda itakuwa haina muhimu. Wajifundishe kazi na tuone wamekuwa wa manufaa. Nimesimama kuunga mkono Hoja hii. Asanteni sana.

Hon. Chiriba: Thank you Mr. Speaker, for this opportunity to register my support to this very important Motion. Maybe Mr. Speaker you can be surprised as to why even pastors can be in support of the Motion on the Floor. I am in support of the same based on the fact that you'll agree with me that problems are inevitable and in as much as we solve inevitable problems, problems will still come. So I have heard even from hon. Members that we look into ways of burying these issues of drugs and whatever. I stand to say that in as much as we stand to say we don't want to see drugs in our county and country, drugs will always be there.

So the issue of coming up with these rehabilitation centres stands to be a very important aspect given that we already have a good number which is already affected and I believe if we have a remedy for that, then a sound mind will have been re-installed and that particular fellow

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

will turn to create employment on the other hand because the same person will turn out to be creative and look into sound ways of making a survival.

I am saying this, if I can even go into Biblical teachings, God made the garden in Eden and in other words, we can say that garden was a place of riches, so there was no lack but there was a simple instruction that man should not eat a certain fruit from that garden but we see how man turned and went ahead to eat from the same. We have practices here under the sun like witchcraft; we have seen men and women who have been alleged to be witches, others being killed, that seeing someone being killed for a certain trend would also serve as a warning for somebody not to tread in that kind of business but even to date, witchcraft is there. So, we cannot stop the issues of drug abuse and that is what made the hon. Member to come up with this Motion.

So, I pray that this Motion will find the favour of this honourable House that it is passed so that we can handle the cases that are currently on and the pieces of advice that we shall be giving the victims, I believe to a certain degree we shall decrease this habit if not abandoning it completely. So I stand to support. Thank you.

Hon. Matsaki: Asante sana Bw. Spika kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kupeana changizo zangu. Mengi yamezungumzwa mazuri kuhusiana na Hoja ambayo iko mbele yetu na nafikiri si jukumu langu la kusema uulize swali lakini naona hata waheshimiwa sioni yule ambaye anaweza kupinga Hoja hii. Nimesimama kuiunga mkono kwa sababu ni kweli vijana wetu wameathirika. Ni jukumu la Bunge kupeana muongozo na muongozo ni kwamba yule waziri anayehusika afanye mikakati ili kwamba zile sehemu ambazo sisi tunazungumzia zijengwe ili vijana waweze kubadilisha tabia zao.

Katika hili Bunge nafikiria Hoja kama hizi ndizo zinazoweza kusaidia vijana wetu. Sisi huwa tunasikia tu vijana ndio viongozi wa kesho; ukianaglia mimi ambaye naoneka hapa ni mmoja katika wale wazee ambao walichaguliwa tena na tumeona mengi. Kuna watu katika Wadi zetu ambao wameharibika ijapokuwa si sana. Mara nyingi kama kiongozi unaposimama na kujaribu kurekebisha vijana, wengine husema uende urekebishe watoto wako.

Wengine huwa wajeuri baada ya kupata zile dawa kwa sababu akili zao huwa si timamu tena. Nimesimama kuunga mkono na pia tukiwa hapa ndani ijapokuwa si moja kati ya hoja lakini ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza Amina mwenzetu ambaye ametajwa katika zile nafasi ambazo wataletwa kupigwa msasa. Nimesimama kuunga mkono hoja hii. Asante sana.

Hon. (Ms.) Radhia: Thank you Mr. Speaker, Sir for giving me this opportunity. I stand to support the Motion on the Floor. We all know that drug trafficking is one of the global menaces with the most complex network. It involves the most influential people in the world; some are politicians, tycoons, business people and they have a kind of network that it is not so easy to break.

I am saddened by the fact that the major responsibility falls on the fault of the National Government because if the National Government was serious to eradicate drug trafficking in the whole country especially in the Coast region, then it would have put the most enforcement to ensure the drug trafficking is eradicated.

I am certain that drug trafficking is going to be there; it will be there and it is still there. I think we understand that the difference between a human being and an animal is mental soundness. The person who abuses drugs; most of these people who uses the hard drugs are not in their mental soundness so eventually it contributes to aggressiveness and this brings about insecurity in our communities. Drug abuse also contributes to some of the sexually transmitted

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

diseases like one of my friends here mentioned that they go hand in hand. Drug abuse also brings about change of sexual behaviours. It has contributed to the rise of homosexuality especially in Malindi.

I was reading an article the other day and it said the HIV spread in Malindi has risen very fast because of homosexuality. Drug abuse also has increased the level of poverty in our community because they are too expensive so instead of someone using the money to educate their children or to contribute to their upkeep, they end up spending the money on the drugs.

Drug abuse also brings about the insanity such that people cannot do anything without them. I would like to suggest that we check on not just coming up with the rehabilitation centres but also coming up with certain recreational centres for our youth because the majority of them who affected by drug abuse are youth.

We can come up with a way of suggesting to the Ministry of Gender and Social Services, Culture and Sports that they equip the recreational centres; they can come up with things like football because there are so many places our youth can go and play so that they can use their excess energy to take part in sports activities instead of diverting that energy to drug abuse.

My fellow hon. Members, I am personally affected because two of my brothers are drug addicts; so standing in front of the House and talking about drug abuse is a personal thing to me. I am affected personally and I know there are some who are affected equally.

I stand to support the Motion on the Floor and kindly also suggest that we check on other ways not just rehabilitation centres but also come up with equipped sports centres so that we can also nurture the talents of our youth. Thank you Mr. Speaker sir.

Hon. Chengo: Asante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii ili nichangie hoja hii. Kwa kweli, namshukuru Mheshimiwa kwa kuleta hoja hii maana hili limekuwa janga. Sehemu nyingi katika Kaunti hii, vijana wengi wameingilia mambo haya na wizi umeongezeka na magonjwa ya zinaa kama tulivyoambiwa na daktari Mheshimiwa Kiraga.

Mara nyingi watu wanapo *abuse drugs* mambo kama haya ya ukimwi na mambo mengine kama wizi yaweze kufanywa kwa kiasi kikubwa. Ombi langu ni kwamba sisi kama wabunge tuweze kupitisha ili Watoto wetu waweze kurekebishwa kwa sababu hali zao zimekuwa ngumu na hata kuwaongoza inakuwa vigumu. Umaskini umezidi kwa sababu wanapotumia hizi dawa hawawezi kufanya kazi.

Kwa hivyo, tukiwasaidia katika hali hii, watoto wetu wataweza kufanya kazi kwa uzuri na tutakuwa na matumaini kwa siku zijazo. Nimesimama kuunga mkono Hoja hii na nasema asante sana.

Hon. Daniel: Asante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii kuchangia. Nilikuwa nikisikiza sana wale vijana wanaokula unga na wale wanaokunywa pombe. Ni kwa nini kijana anaenda kula unga ama pombe? Nimefuatilia haya mambo na sio kwamba hawa vijana wanakula kupenda bali ni kwa sababu hawana ajira. Na utakuta waheshimiwa wengi wanakosa kuwawezesha wale vijana na wanabaki vile vile.

Kwa hivyo, tukisema tunaenda kujenga hizi zahanati ili vijana tuwaweke pale, tutajenga kweli lakini kama hatutaweza kuwawezesha vijana kupata kazi, hatutakuwa tumewasaidia. Asante Mheshimiwa Spika.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Speaker (Hon. Kahindi): In the absence of any other business, I move to adjourn the House until in this afternoon.

The House rose at 11:00 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*